

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),
S.L.P 02,
USHIROMBO
BUKOMBE

MKOA WA GEITA:

Simu: 028 2520709
ded@bukombedc.go.tz



TAARIFA KWA UMMA

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe inapenda kuwatangazia wananchi wote wa Wilaya ya Bukombe kuwa **Ndugu Amon Kafiriti** ndiye **AFISA MALALAMIKO** wa Wilaya ya Bukombe. Afisa Malalamiko atashughulikia malalamiko yote ya Watumishi na Wananchi kwa ujumla .

Lengo Kuu la kuanzishwa utaratibu huu ni kuimarisha ubora wa huduma zinazotolewa na ubora wa huduma hizo unaweza kuimarisha kwa kuondoa mambo yanayofanya huduma zilalamikwe, kujenga mauhusiano bora baina ya wananchi na taasisi za umma na kuwezesha taasisi kupata mrejesho wa huduma wanazotoa kwa wananchi zimepokelewaje.

Afisa Malalamiko ana jukumu la Kupokea na kushughulikia malalamiko kwa wakati ili kuwaridhisha wale wanaohudumiwa, Kukuza mtazamo wa kuwajali wananchi ambao ndiyo wateja kwenye Taasisi za umma ili waridhike na waendelee kutumia huduma zinazotolewa., pia Kukuza uwajibikaji wa watumishi wa umma kwa wananchi(wateja) kwa kuwa mrejesho wa wananchi utaanisha mahitaji ya wananchi na pia utatumika kuweka mikakati ya kuimarisha ubora wa viwango na huduma zinazotolewa, Kuongezeka kwa uwazi na shughuli za Taasisi kueleweka kwa urahisi.

Aidha Afisa Malalamiko atazingatia utunzaji wa siri wa mlalamikaji au mtoa kero na malalamiko yatashughulikiwa na kuhifadhiwa kwa usiri unaostahili, na mchakato wa kushughulikia malalamiko hayo utakuwa wazi,unaoeleweka kwa wadau wote na utatoa fursa ya maamuzi kuhojiwa katika ngazi yoyote, pia mlalamikaji atapatiwa ufumbuzi wa lalamiko lake pale pale alipolalamika na ikilazimu kupeleka lalamiko hilo mahali pengine mchakato wa kushughulikia lalamiko lake hautachukua muda mrefu.

Maelekzo ya kuasilisha lalamiko au kero kwa Afisa Malalamiko wa Wilaya ni kwa **kupitia sanduku la maoni , namba ya simu 0622-295619 , au kufika ofisi ya Ustawi wa Jamii** iliyopo Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe.

Imetolewa na;
Tusa D Mwambenga
Afisa Habari na Uhusiano
23/02/2017
BUKOMBE

